

4.0 Kilimo cha Karanga

Ili kuweza kupata mavuno mengi na yaliyo bora, ni muhimu sana kuzingatia kanuni za kilimo bora cha zao hili kama:

Kuhifadhi mbegu za kupanda katika maganda yake.

Kupanda kwa wakati mwishoni mwa Desemba hadi katikati ya Januari na nafasi sentimita 10 kati ya mmea na mmea na sentimita 50 kati ya mstari mmoja hadi mwingine.



Kupalilia kwa wakati unaofaa .

Kuzuia mashambulizi ya wadudu na magonjwa.

Wadudu kama mafuta wanaweza ku-zuiliwa kwa kupanda mapema, kupanda karibukaribu, kuchanganya karanga na mazao mengine.

Funza (buu)




Wadudu mafuta kwenye karanga



Kuna magonjwa mengi yanayoathiri zao la kama vile madoa ya majani na kutu, ugonjwa wa kuoza na ugonjwa wa rosette. Unaweza kuyazuia kwa kutumia madawa na usafi wa wa shamba.

Ugonjwa wa rosette 'Ukoma'



Ugonjwa madoa ya majani



Kutu ya majani

TAASISI YA UTAFITI NA MAFUNZO KANDA YA KUSINI



KILIMO BORA CHA KARANGA



Kimetayarishwa na :

Taasisi ya Utafiti Naliendele,

Mradi wa Karanga/McNight Foundation,

S.L.P. 509,

MTWARA

Juni 20

Utangulizi

Katika Tanzania, Karanga hustawi zaidi Mikoa ya Mtwara, Dodoma, Shinyanga na Tabora. Zao hili ni maarufu sana kwa kutoa mafuta.

Karanga hutumika kama chakula cha binadamu. Mashudu na majani yake ni bora sana kwa kulishia wanyama. Karanga pia hurutubishia ardhi.

Uzalishaji wa zao hili bado upo chini mno kutokana na sababu mbalimbali kama kutokufuata kanuni za kilimo bora.

2.0 Mazingira yanayofaa

Karanga hustawi vizuri katika maeneo yenye mwinuko chini ya mita 1500 toka usawa wa Bahari na mvua ya wastani wa milimita 1000 kwa mwaka. Udongo mzuri kustawisha karanga ni ule wa kichanga wenye kupenyeza maji kirahisi. Sehemu zenye udongo wa mfinyanzi na zinazotuamisha maji hazifai kulima zao hili.

3.0 Aina za Karanga

Kuna aina sita za mbegu bora za karanga ambazo zimefanyiwa utafiti na kutolewa mapendekezo na wakulima. Mbegu hizi zinakubalika kwa wakulima na masoko

3.1 Pendo

Huchukua wastani wa siku 90 mpaka 100 toka kupanda hadi kukomaa. Mbegu zake zina rangi ya udongo. Hutoa mavuno kiasi cha kilo 1500 kwa hekta.



3.2 Naliendele 2009.

Mbegu ya muda mfupi. Huchukua siku 90 mpaka 100 kukomaa. Huzaa wastani wa kilo 1000 kwa hekta.



3.3 Mangaka 2009

Hukomaa kwa siku 90 mpaka 100. Huzaa mbegu 2-3 kwenye kitumba kimoja. Hutoa wastani wa kilo 1500 kwa hekta.



3.4 Mnanje 2009

Huchukua siku 110 mpaka 120 toka kupanda hadi kukomaa. Mbegu zake ni kubwa zina rangi nyekundu. Mnanje hutoa mavuno ya wastani kilo 1000 kwa hekta.



3.5 Masasi 2009

Huchukua siku 110 mpaka 120 toka kupanda hadi kukomaa. Mbegu zake ni kubwa, nyekundu. Hutoa mavuno ya wastani kilo 1000 kwa hekta. Zina-vumilia ugonjwa wa ukoma.



3.6 Nachingwea 2009

Aina hii ya mbegu huchukua siku 110 mpaka 120 toka kupanda hadi kuvuna. Mbegu zake zina saizi kubwa. Hutoa kiasi cha tani moja kwa hekta. Zinzvumilia ugonjwa wa ukoma.

